



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU
WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA
Mazishi ya Kitaifa ya Hayati Mwai Kibaki, Rais wa Awamu ya Tatu wa
Jamhuri ya Kenya**

**NAIROBI KENYA
TAREHE 29 APRILI, 2022**

Mheshimiwa Uhuru Muigai Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya;
Mheshimiwa William Rutto, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Kenya;
Mheshimiwa Martha Koome, Jaji Mkuu wa Kenya;
Mheshimiwa Mama Margaret Kenyatta, Mke wa Rais wa Jamhuri ya Kenya;
Familia ya Hayati Rais Mwai Kibaki;
Waheshimiwa Mawaziri;
Waheshimiwa wabunge;
Waheshimiwa Viongozi wote wa Serikali mliopo;
Waheshimiwa Viongozi wa madhehebu yote ya dini mliopo;
Wananchi wote wa Jamhuri ya Kenya; na
Wageni wote waliofika kuungana na Wakenya kwenye mazishi haya ya Kitaifa.

Awali ya yote, naomba niwasilishe kwako, Mheshimiwa Rais Uhuru Kenyatta, na kupitia wewe kwa Serikali, Familia ya Hayati Mwai Kibaki pamoja na Wananchi wa Jamhuri ya Kenya, salamu za pole kutoka kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali na wananchi wote wa Tanzania. Mheshimiwa Rais Samia pamoja na watanzania wote tulipokea kwa huzuni kubwa taarifa ya kifo cha Rais Mstaafu Mwai Kibaki. Mheshimiwa Rais Samia alipenda sana kuwepo hapa na kumshukuru Mungu pamoja nanyi kwa maisha ya Hayati Mwai Kibaki, lakini kwa sababu zilizokuwa nje ya uwezo wake haikuwezekana na hivyo amenituma nimuwakilishe.

Nimeambatana na Mheshimiwa Kanali Mstaafu Abdulrahman Kinana, Makamu Mwenyekiti wa Chama Tawala CCM, ambaye alipokuwa Spika wa Bunge la Afrika Mashariki alifaya kazi kwa karibu na Hayati Mwai Kibaki. Rais Samia na Watanzania wote tunawaombea faraja familia ya Mwai Kibaki na pia umoja, amani na maendeleo ya kweli wananchi wa Kenya mambo ambayo Hayati Mwai Kibaki aliyasimamia wakati wa uhai wake.

Mheshimiwa Rais, Familia ya Kibaki, Wageni na Wakenya wote;
Hayati Mwai Kibaki alikuwa na uwezo mkubwa, maono na kipawa cha uongozi. Historia yake inaonesha kuwa alikuwa bingwa kuanzia shule na vyuo vikuu vyote alivyosoma. Aliaminiwa na Marais wote wa Kenya kabla yake na

kuitumikia Jamhuri ya Kenya kwa moyo thabiti katika nafasi za Uwaziri, Ubunge, Makamu wa Rais na hatimaye Rais wa Tatu wa Kenya. Atakumbukwa sana kwa kuwa Mwanasiasa mahiri na kinara wa demokrasia ya vyama vingi hapa Kenya na kwa mchango wake mkubwa katika kuboresha maisha ya wananchi wa Kenya kwa kuimarisha uchumi, kuboresha elimu na huduma mbalimbali za kijamii. Hakika Watanzania tulijifunza mengi kutokana na uongozi wake.

Kwetu sisi Watanzania, Hayati Rais Mwai Kibaki alikuwa ni rafiki. Wakati wa uongozi wake, aliendeleza na kuimarisha ujirani mwema na ushirikiano wa kindugu na kihistoria baina ya Tanzania na Kenya. Kwa kutambua mchango wake katika kuendeleza undugu wetu, mwaka 2013 alipofanya ziara nchini Tanzania, tulimpa heshima aliyostahili ikiwa pamoja na kubadilisha jina la iliyokuwa barabara ya *Old Bagamoyo* na kuiita "**Barabara ya Mwai Kibaki**" kama kumbukumbu.

Mheshimiwa Rais, Familia ya Kibaki, Wageni na Wakenya wote;

Pamoja na mambo mengi aliyoyafanya ndani na nje ya Kenya, juhudzi za Hayati Rais Mwai Kibaki katika kuimarisha Jumuiya ya Afrika Mashariki haziwezi kusahaulika. Hayati Mwai Kibaki alichaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Kenya mwaka 2002 wakati Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa na miaka miwili (2) tu tangu ilipoanzishwa tena mwaka 2000. Hayati Rais Kibaki atakumbukwa kwa kukuza na kuimarisha Mtangamano wa Jumuiya yetu, kuhimiza matumizi ya lugha ya Kiswahili na kwa juhudzi zake za dhati katika kuhakikisha Sheria na Mikataba mbalimbali inapitishwa kwa maslahi mapana ya Jumuiya yetu. Hayati Rais Kibaki aliunga mkono kwa nguvu zote mikataba ya kuimarisha biashara na uhuru wa watu kutembea kati ya nchi zetu, hatua ambayo imetuwezesha kuimarisha ujirani na undugu wetu hadi leo. Aidha, katika kipindi cha uongozi wake kama Mwenyekiti wa Jumuiya, ndio wakati nchi wanachama ziliongezeka baada ya Jamhuri za Rwanda na Burundi kujiunga mwaka 2007. Hakika kama Jumuiya tumejifunza mengi sana kutoka kwake.

Mheshimiwa Rais, Familia ya Kibaki, Wageni na Wakenya wote;

Watanzania tutaendelea kumkumbuka Hayati Rais Mwai Kibaki kama nyote inayong'aa na mwamba imara wa maendeleo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tushirikiane kumwombea Hayati Rais Mwai Kibaki roho yake ipumzike kwa amani. **Amina.**

Asante sana Mheshimiwa Rais.